



TAARIFA KWA UMMA UHALALI WA VYETI VYA KUZALIWA VINAVYOJAZWA KWA MKONO

Serikali imeanza maboresho ya mfumo wa Usajili wa matukio muhimu ya binadamu ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kusajiliwa na kupata vyeti vya uthibitisho wa kutokea matukio hayo. Maboresho haya yanatekelezwa kupitia Mkakati wa Usajili wa matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu (Civil Registration and Vital Statistics - [CRVS] Initiative) ambao unatoa suluhisho kwa changamoto mbalimbali zinazosababisha wananchi wengi kushindwa kusajiliwa ikiwa ni pamoja na umbali mrefu kati maeneo ya makazi ya wananchi na Ofisi za usajili.

Utekelezaji wa Mkakati huu umeshaanza kwa kundi ka watoto kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto walio na Umri Chini ya Miaka Mitano (Under Five Birth Registration Program) unaotekelezwa katika mikoa Saba ya Tanzania bara ambayo ni Mbeya, Songwe, Mwanza, Iringa, Njombe, Geita na Shinyanga. Katika mikoa hii, watoto wote walio na umri chini ya miaka mitano wanasajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa **VINAVYOJAZWA KWA MKONO** bila malipo katika Ofisi za Watendaji Kata na Vituo vya Tiba vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto na taarifa za aliyesajiliwa kutumwa kwa njia ya mtandao na kuingia moja kwa moja katika kanzidata ya RITA.

Napenda kuutaarifu Umma kwamba Cheti cha Kuzaliwa kilichojazwa kwa mkono ni cheti halali kama ilivyo kwa vilivyochapishwa kwa mashine hivyo vinaweza kutumika mahali popote kupata huduma inayohitajika.

Msajili Mkuu wa Vizazi na Vifo ndiye mwenye dhamana na mamlaka ya kutoa vyeti vya kuzaliwa ikiwa ni pamoja na kuvihakiki na kuvithibitisha uhalali wake. Hivyo nazisihi Taasisi zote nchini kuvikubali vyeti hivi mara vinapowasilishwa kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali. Endapo Taasisi hizo zina mashaka na vyeti hivyo na zinahitaji ufafanuzi au uthibitisho wa vyeti vilivyowasilishwa, zisisite kuwasiliana na Ofisi za RITA na siyo kuvikataa na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Natoa rai kwa wananchi wote kuendelea kusajili na kupata Vyeti vya Kuzaliwa kwa utaratibu uliopo katika eneo analoishi kwa manufaa yao wenyewe na nchi kwa ujumla.

Emmy K. Hudson

**Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu/ Msajili Mkuu wa
Vizazi na Vifo**